JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

BARAZA LA FAMASI

TAARIFA MUHIMU

DODOMA: 26 Novemba, 2026

Tunapenda kuwataarifu Watarajali wote waliochagua vituo vya mafunzo kwa vitendo kwa mwaka 2026/2027 kuwa barua za kuripoti na kuanza mafunzo katika vituo zitatolewa kupitia Ofisi za Kanda za Baraza la Famasi.

Hivyo, Watarajali waliochagua vituo na kusajiliwa wanaelekezwa kuanzia **tarehe 27 Novemba,2026** kufika katika Ofisi za Kanda kulingana na Mkoa wa kituo alichochagua kwa ajili ya kuchukua barua na kuripoti kwenye vituo vya mafunzo.

Aidha, Watarajali wanakumbushwa kuwa wanapaswa kuripoti kwenye kituo cha mafunzo ndani ya **siku 5** kuanzia tarehe **01 Desemba, 2026**.

Ofisi za Kanda za Baraza la Famasi na Mikoa ya vituo vya mafunzo ni kama zilivyoainishwa hapa chini;

S/N	Kanda	Mikoa ya Vituo vya Mafunzo
1.	Kanda ya Kati	Dodoma, Singida, Iringa, Morogoro na Tabora
2.	Kanda ya Mashariki	Dar es Salaam, Pwani na Mtwara
3.	Kanda ya Ziwa	Mwanza, Geita, Kagera, Shinyanga, Mara, Simiyu, Shinyanga, Katavi na Kigoma
4.	Kanda ya Kaskazini	Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga
5.	Kanda ya Nyanda za Juu Kusini	Mbeya, Songwe na Ruvuma

Imetolewa na;
Msajili,
Baraza la Famasi,
DODOMA.